# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu




3/2025

*a publication of* ***Assemblies of Yahweh***

THE SACRED NAME BROADCASTER

*An **Assemblies of Yahweh** publication.*
***Assemblies of Yahweh**, **The Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***March 2025***
***Volume LVI, Number 12***

# YALIYOMO


Page 1


Page 10


Page 17


***1.*** ***Messiah katika Agano la Kale, Sehemu ya 5***

*Fundisho la Agano Jipya la Messiah linathibitishwa kutoka kwa mafundisho ya Agano la Kale, ambayo yanaunda msingi wa Imani yetu.*

***5.*** ***Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa, Sehemu ya 5***

*Mwenye-enzi Yahweh aliumba madarasa manne ya viumbe ili kumtumikia Yeye. Basi tuhakikishe kwamba hatulegei kamwe katika kujitolea kwetu kama walivyofanya wengine*

***10.*** ***Mwelekeo wa Kinabii: Vita, Njaa na Matetemeko ya Ardhi***

*Yahweh anatupea dirisha nyembamba la wakati kufanya kuitwa kwetu na kuchaguliwa hakika.*

***17*** ***Mapishi ya siku za mikate Isiyotiwa chachu***

*Sikukuu ya Mikate isiyotiwa Chachu ni wakati maalum sana wa mwaka! Yahweh ametupea chakula kitamu, safi na kisichotiwa chachu kula, ambacho hakina chachu.*


## Jalada Letu

*Kila Pasaka, tunakumbuka mateso na kifo cha Mwokozi wetu Yahshua aliye Messiah. Taji la miimba, kuteswa kwa mjeledi wa Warumi, na misumari ya chuma kupitia mikono yake na miguu yake- Yahshua aliteseka katika uchungu kwa sababu ya dhambi zetu.*




***"Kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, akahesabiwa pamoja na hao wakosao, walakini alichukua dhambi za watu wengi, na kuwaombea wakosaji."*** *(Isaya 53:12b) Yahshua alitoa ishara moja pekee- siku tatu na kucha tatu kaburini- kwamba alikuwa Messiah. Yahshua alilazwa katika kaburi la mtu tajiri (Isaya 53:9) na kufufuka katika mwisho wa sabato. ( Mathayo 28:1)*

*Jalada la mwezi huu limechukuliwa ndani ya Kaburi la Bustani (karibu na Golgotha-mahali pa Fuvu la Kichwa) ukiangalia nje. Mwenyewe wa Kaburi la Bustani amechonga tangazo la malaika (Mathayo 28:6, Mariko 16:6, na Luka 24:6).* ***"Hayupo hapa, kwani amefufuka,"*** *kwenye mlango wa kaburi.*

*Leo, Yahshua yuko kwenye mkono wa kuume wa Yahweh, karibuni atatelemka kuanzisha Ufalme wa Yahweh duniani. Uko tayari kwa Kurudi mara ya Pili kwa Yahshua?*

Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenzi wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.

© Hakimiliki 2024 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.
Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.

***Mwanzilishi na Mwandishi:** Mzee Jacob O. Meyer*



# Messiah katika Agano la Kale

Na Mzee Jacob O. Meyer

Yale watu wengi hivyo wa ukr-sto wa kawaida wa kisasa hawatambui ni kwamba Biblia ni kitabu cha unabii. Hili linaifanya Biblia ya kufaa kwa watu wa zama zote. Nyuma kabisa katika bustani la Edeni, wakati Adamu na Hawa walifanya dhambi kwanza, Mwenye-nguvu Yahweh aliwaahidi Mwokozi. Alisema kwamba mbegu ya mwanamke ingeponda kichwa cha nyoka. Ahadi ilikuwa unabii. Mwenye-nguvu Yahweh hakumtuma aliye Messiah mara moja. Hakumtuma Mkombozi kununua tena watu Wake katika kipindi hicho hasa. Hata hivyo, unabii ulifanywa, na ulikuwa hakika kutimizwa katika tarehe fulani wakati ujao. Siku moja, wakati Messiah anarudi, kichwa cha nyoka (Shetani) kitapondwa. Angalia Warumi 16:20.

Unabii katika Biblia ndio unaoifanya iwe hai kwetu leo- katika wakati wetu. Tunagundua kwamba wakati wowote tunaangalia kwa gazeti leo tunaweza kuona ulimwengu ukizama hata zaidi kwenye shimo la uovu na dhambi. Mtu anahitaji tu kuchukua gazeti, na anaweza kusoma ripoti za vurugu, mauaji, ubakaji, wizi, na aina yote ya uovu mwingine. Unabii unatuambia kwamba siku za mwisho zitakuwa tu kama siku za zama za Nuhu, ni kama tu Mtume Paulo anavyotabiri katika 2 Timotheo 3:13 kwamba, ***"Lakini watu wabaya na wadanganyi wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika."*** Soma mlango mzima na utambue unabii wote anaofanya Paulo.

Mtu anayesoma Biblia anaweza kusema kutoka kwa unabii huu kwamba kwa kweli tuko katika siku za mwisho. Tunapohitimisha kwamba ulimwengu kweli uko katika siku za mwisho, tutatayarisha maisha yetu ili kwamba tunaweza kuwa kama Yahshua kwa kutunza Sheria za Yahweh. Tunao huo motisha ulioongezewa kutayarisha maisha yetu ili kwamba tunaweza kusimama salama katika siku ya mabaya wakati dhiki itashambulia.

Mwenye-nguvu Yahweh ametabiri mambo haya kwa Roho Wake Mtakatifu. Manabii Wake (watumishi Wake) wameyarekodi kwetu. Roho Mtakatifu uliwaongoza watu hawa kuandika unabii huu ili kwamba watu wa Yahweh wangekuwa na nafasi kujitayarisha wenyewe dhidi ya siku ya mabaya. Lazima tutambue Biblia kama kitabu maarufu cha unabii kinachoonyesha jinsi binadamu alikataa serikali ya Mwenye-nguvu Yahweh, lakini siku moja serikali hiyo itachukua utawala wa dunia hii, na, kisha, dunia hii itatawaliwa katika haki.

***Fundisho la Messiah linakuja kwetu kutoka kwa utamaduni wa Waisraeli, sio kutoka kwa dhana ya upagani. Yahshua aliye Messiah Mwenyewe alitabiriwa nyuma kabisa katika historia wakati Adamu na Hawa walipofanya dhambi.***

Katika sehemu hii ya msururu wa sasa, tunataka kuanza ujumbe kwa kusoma Amosi 3:7. Wakati wowote chochote kinafanyika duniani cha matokeo makubwa, lazima tuamini kwamba Mwenye-nguvu Yahweh alikuwa awali amerekodi unabii unaohusiana nacho mahali fulani katika Neno Lake. Tambua nini tunapata katika Amosi 3:7. ***"Hakika Mwenye-Enzi Yahweh hatafanya lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake."*** Manabii wa Yahweh wanarekodi utabiri huu mbele ya wakati kupitia kwa ufunuo uliotolewa kutoka Juu na Roho Mtakatifu. Mwenye-nguvu Yahweh alitaka kuonya mapema watu Wake, na hivyo, kuwatayarisha wao mbele ya wakati.

Ruhusu tuzingatie juu ya Messiah sasa. Watu wengi hivyo wanaamini kwamba Agano Jipya linajumuisha chombo kilichojitenga kabisa, tofauti kabisa kutoka kwa Maandishi ya Agano la Kale. Watu wengi katika Ukr-sto wa kawaida leo wanahisi kwamba wanaweza kuondoa Agano la Kale kutoka kwa Biblia, na hawangepoteza chochote; hata hivyo, dhana hii ni ***yenye makosa***.

Unajua kwamba kunao karibu vifungu 287 tofauti vilivyonukuliwa moja kwa moja kutoka kwa Agano la Kale? (baadhi vimerudiwa). Hii ni la faraja kabisa kwa watu ambao wanajua kwamba Agano Jipya lazima liwe na msingi mahali fulani. Kusikitisha, kwa karne watu hawajatambua kwamba msingi wa Agano Jipya umewekwa katika Agano la Kale.

Watu wengi wamepotoka kwa mijadala mbalimbali, wakianzisha mafundisho ambayo hayawezi kuthibitishwa-hata mafundisho ambayo yako katika makosa kabisa. Kama wangeweza kufikia kwa hitimisho kwamba Agano la Kale ni msingi wa Imani yetu, na kwamba Agano jipya linakamilisha mpango wa wokovu uliotabiriwa katika Biblia ya Kiebrania, basi ingekuwa haiwezekani kabisa hivyo kwamba wangeweza kupotoka kwa Njia Nyembamba. Mkanganyiko wa mafundisho ambao ni dhahiri hivyo kwenye wigo wa Ukr-sto leo ungepungua. Ukr-sto leo unaunga mkono mengi ya mafundisho, lakini kunalo tu, fundisho moja la kweli, na hilo ndilo sote tunapaswa kujitahidi kujifunza! Fundisho la kweli la Yahweh linaweza kupatikana kwa kusoma Biblia- kuitafiti na kuioanisha kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Tunapoielewa Biblia katika usanidi huu, basi tutakuwa tumefanya hatua kubwa kwa mara nyingine tena kuelekea kwa kumrudi Mwenye-nguvu Yahweh katika kweli na kurejesha Ibada safi ya kusanyiko la Kitume.

Lazima tukumbuke *sitz im leben* (ambayo inamaanisha mpangilio wa maisha) ya Agano Jipya.

Mpangilio wa maisha wa Agano Jipya ulikuwa wenye mzizi wa utamaduni wa Waisraeli-utamaduni wa Kiyahudi, watu wa Kisemitiki. Kiini chake kilikuwa mafundisho safi ya utunzaji wa amri. Haiwezi kupatikana katika lugha ya Indo-Ulaya, au yoyote ya utamadani wa upagani wa Wagiriki au mithilojia ya Warumi. Kinyume chake, mpangilio wa maisha wa Agano Jipya ni wenye msingi wa ndani katika ibada ya Waisraeli-Waebrania. Tunapofika kwa ufahamu huo, basi tunafikia hatua ya msingi ya kurejesha mafundisho ya kweli ya kusanyiko la Kitume.

Vivyo hivyo, fundisho la Messiah linakuja kwetu kutoka kwa utamaduni wa Waisraeli, sio kutoka kwa dhana ya upagani. Yahshua aliye Messiah Mwenyewe alitabiriwa nyuma kabisa katika historia wakati Adamu na Hawa walipofanya dhambi. Hilo lilikuwa takribani miaka 6,000 iliyopita.

Walipokuwa katika Bustani la Edeni, wakati Mwenye-nguvu alimweka Adamu na Hawa katika mazingira mazuri ambayo yalikuwa ya kufaa kwa uendelezaji wa maisha yao, wazazi wetu walifuzwa njia za Aliye Juu. Edeni palikuwa mahali pazuri, pazuri kuwa napo kama nyumbani, kuishi kama makaazi yako. Walakini, Adamu na Hawa hawakuwa na heshima ya kweli kwa upande wa Mwenye-nguvu Yahweh. Walikataa amri Zake, na, kama matokeo yake, wakaasi dhidi ya serikali Yake. Walikubali serikali na utawala wa Shetani Ibilisi. Kama matokeo yake, Mwenye-nguvu Yahweh aliwaadhibu kwa kuwaendesha kutoka kwa Bustani la Edeni. Kisha walilazimishwa kupata mtindo wa maisha ambao kamwe hakukusudia kwao.

Walakini, wakati walifanya dhambi, aliwaahidia Mwokozi! Ahadi hiyo inapatikana katia Mwanzo 3:15. Ni unabii uliorekodiwa wa kwanza wa Messiah. ***"Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake, huo utakuponda kichwa, na wewe utamuumiza kisigino."***

Utabiri huo unafuatia njia yote ya historia ya Biblia. Messiah anaelezewa katika unabii mbalimbali, kama vile Mika 5:2. Tunajifunza kutoka kwa kifungu hiki haswa ni wapi aliye Messiah alitabiriwa kuzaliwa. "***Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele***."

Hapa katika kifungu hiki, tunapata kwamba Yahshua aliye Messiah angezaliwa katika Bethlehemu. Katika Kiebrania, jina *Bethlehemu* linamaanisha *nyumba ya mkate*. Ni wapi Herode aliwatuma *magoy* (mamajusi)? Aliwatuma Bethlehemu, na katika Bethlehemu walimpata Messiah. Vipi walijua ni katika mji upi watatafuta kupata mahali pa kuzaliwa pa Messiah? Herode aliwauliza baadhi ya wasomi na wanafunzi wa siku zake kuhusiana na Messiah na wasomi wa Biblia mara moja wakamwarifu kwamba Messiah alitabiriwa kuzaliwa katika Bethlehemu; kwa sababu hiyo, wakaenda Bethlehemu.

Ingawa unavyoonekana ni usio na maana, mji huu mdogo ulipangwa kuwa mahali pa kuzaliwa pa Messiah. Kutoka kwake alitokea mfalme Daudi, mtu aliyefanya kazi kuunganisha makabila 12 ya Israeli kwenye kitengo kilichoshikamana, Vivyo hivyo, Messiah wa Israel ataunganisha mataifa ya ulimwengu kwenye kitengo cha kiserikali kilichoshikamana, ufalme wa Yahweh. Unaona usambamba na muungano hapa? Usambamba ni dhahiri tunapozingatia unabii wa Isaya 9:6-7. **"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake: naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, El Mwenye-nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na Mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake, kuuthibitisha na kuutegemeza, kwa hukumu na kwa haki tangu sasa na hata milele. Bidii ya Yahweh wa majeshi ndio itakaotenda hayo."** Yahshua aliye Messiah alitimiza unabii wa Mika. Alizaliwa katika Bethlehemu, ingawa wazazi wake hapo awali walikuwa wameenda Nazareti. Baadaye, mara nyingine tena walihamia Nazareti. Na hapo Yahshua alilelewa, katika mazingira ya Nazareti.

Basi tuangalie kwa Andiko lingine. Geukia kwa Mathayo mlango wa 1, ambapo tutapata kwamba Messiah ametabiriwa kuzaliwa na bikira.***"Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; ambayo inatafsiriwa, Elohim pamoja nasi."*** (Mathayo 1:23). Hii ni nukuu la moja kwa moja kutoka Isaya 7:14.

Tunapochambua kifungu hiki cha Maandiko, tunapata kwamba Messiah alitabiriwa kuzaliwa na bikira. ***"Kwa hiyo Yahweh mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli."*** Watu mbalimbali wa kihakiki wamenyima sifa Andiko hili kama unabii wa Messiah. Lakini tusiwe wenye haraka sana katika kukataa kwetu kwa andiko hili.

Kwanza kabisa, wataashiria kwamba neno *bikira* hapa limetafsiriwa kutoka kwa neno *'almah*, ambalo tunakubali kwa urahisi kuwa sahihi. Neno *'almah* linaonekana hapo, na sio neno la kawaida la Kiebrania kwa bikira, ambalo ni *bethulah*. Walakini, kabla turuke kwa hitimisho, ruhusu tutambue kwamba kuzingatia kwa kila tukio ambapo neno *'almah* linaonekana katika Biblia ya Kiebrania itatuarifu sisi kwamba neno linatumika kwa **bikira KIJANA**. Neno *bethulah* linaweza kumaanisha bikira wa umri wowote, lakini neno *'almah* basi lazima linamaanisha BIKIRA WA UMRI MDOGO. Mwandishi angependekeza ufafanuzi huu.

Katika Kuongezea, wanathiolojia hao huria ambao wanakataa kuzaa kwa bikira lazima wakabiliwe na tafsiri ya Kigiriki ya **Septuagint** ya kifungu hiki. ***"Kwa hiyo*** [Yahweh] ***mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, nawe utamwita jina lake Imanueli. Siagi na asali atakula, kabla ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema. Kwa maana kabla mtoto huyo hajajua kuyakataa mabaya na kuyachagua mema, nchi ile, ambayo wewe unawachukia wafalme wake wawili, itaachwa ukiwa."***

Katika toleo hili la Kigiriki la **Septuagint** neno *parthenos* linapatikana. Neno la Kigiriki *parthenos* hakika linamaanisha *bikira*. Ni Wayahudi ambao walitafsiri Isaya 7:14-16 kutoka kwa Kiebrania hadi kwenye **Septuagint** ya Kigiriki karibu miaka 225 kabla ya kuzaliwa kwa Messiah. Kwa hivyo, waumini wa Kitume, waumini wa kimessiah wa zama za kitume, walikabili wakosoaji wao kwa hitimisho hilo: "Mliitafsiri bikira, na hilo ndilo hasa nini neno *'almah* linamaanisha."

Ikiwa hujawahi kutambua uzuri mkubwa, mshikamano na uthabiti wa nakala ya Maandiko Matakatifu, unaweza kutambua ukweli huu kwako mwenyewe kwa kurudi nyuma kwa sahihi halisi za asili, kwa ukaribu uwezavyo kurudi kwazo, na kwa lugha ya asili ambayo Biblia iliandikwa, kusuluhisha shida za mafundisho ya Biblia. Kama sivyo, basi unaweza kukosa moja ya kipengele kikubwa cha kusoma Biblia. Sisi katika Assemblies of Yahweh, tumegundua Jina Takatifu la Mwenye-nguvu Yahweh na Jina la Kweli la Mwokozi ambalo lilikuwa Yahshua Hamashiach, Yahshua aliye Messiah. Haya ni mambo machache muhimu ambayo tumeweza kugundua kwa kurudi kwa hati za asili.

Jiunge nasi mara kwa mara kwa utafiti wa kutia msukumo wa Neno la Yahweh. Kamwe hautajutia wakati utakaotumia kwa Neno la Yahweh! SNB

***Ikiwa hujawahi kutambua uzuri mkubwa, mshikamano na uthabiti wa nakala ya Maandiko Matakatifu, unaweza kutambua ukweli huu kwako mwenyewe kwa kurudi nyuma kwa sahihi halisi za asili, kwa ukaribu uwezavyo kurudi kwazo, na kwa lugha ya asili ambayo Biblia iliandikwa, kusuluhisha shida za mafundisho ya Biblia.***





# Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa

SEHUME YA 5

**Na Mzee Jacob O. Meyer**

Ni kwa nini Ukr-sto wa kidunia, kwa karne zilizopita haujahubiri kusudi lote la Neno La Yahweh? Jibu ni kwamba ukr-sto wa kidunia kwa kweli umekata Biblia katika vipande viwili, kwa kiasi fulani zaidi ya nusu, kwani Agano la Kale linajumuisha nyenzo nyingi kuliko Agano Jipya. Biblia lazima izingatiwe kwa usahihi kama kitengo kimoja, juzuu moja, kazi moja.

Tunasoma katika Matendo ya Mitume 20:27 kwamba Mtume Paulo anaelezea kwamba hakupuuza kuhubiri "kusudi lote" (ujumbe mzima) wa Maandiko Matakatifu. Biblia sio ujumbe usiounganishwa; kwa hivyo, ili kuelewa usahihi, mwanafunzi wa Biblia lazima asome na kutumia Maandiko Matakatifu kutoka Mwanzo hadi Ufunuo.

Geukia kwa Isaya 28:9, ***"Atawafundisha nani maarifa? Atamfahamisha nani habari hii? Je! Ni wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini? Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo. "***

Nabii Isaya anatufundisha kutumia Biblia nzima. Ukweli wa kibiblia unapatikana ukiingiliwa kupitia kwa nakala nzima, "*huku*

*kidogo na huku kidogo*." Kwa sababu hiyo, tunapaswa kusoma mada kote kabisa katika Biblia, kutoka Mwanzo hadi kitabu cha Ufunuo. Katika nakala ya Kiebrania ya Isaya 28, tunakutana na wimbo mdogo ambao uliundwa katika mifumo ya shule ya Israeli ya kale. Nakala ya Kiebrania inasoma: "*zav le zav, zav le zav, chav le chav, chav le chav, zeer sham, zeer sham*." Walakini, wimbo huu mdogo unayo maana. Sio tu kuhimiza watoto kuimba wimbo kwa pamoja; badala yake, inanuiwa kuvutia juu ya watoto wote wa shule za Israeli (na pia watu wazima) kwamba Biblia lazima izingatiwe kama inayoweka mbele ujumbe mmoja kamili. Kote katika juzuu utapata marejeleo na maelezo kwa mada hizi mbalimbali na maneno. Endelea katika Isaya 28:11, ***"La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa; ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika, lakini hawakutaka kusikia-***[inaonekana kwamba watu hawataki kusikia chochote isipokuwa yale wanalenga wenyewe kuamini***] kwa sababu hiyo neno la Yahweh kwao litakuwa hivi, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo; ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa.***"

Vipi tutafikia mafundisho safi? Wanathiologia wa kuhafidhina, ambao wanafunza njia sahihi ya kusoma Biblia, wanatambua Biblia kama kitengo kamili. Hii ndio njia ya kusoma Biblia wanayofunza katika seminari; hata hivyo, wakati mwingi, shida ni kwamba hawapokei ushirikiano katika matumizi ya vitendo. Biblia katika dini ya kidunia, haitambuliwi kama kitengo kamili. Inatambuliwa tu kama, labda, kitabu cha msukumo kilicho na vifungu fulani vya kutia msukumo, kama vile kitabu cha Zaburi, Mahubiri juu ya Mlima, au vifungu sawa. Kwa kweli, hiki ni kitabu chenye unabii, maagizo, mafundisha, na kinaweka nje kiwango cha kupata maisha yenye furaha na yenye matunda. Viwango hivyo ni vilivyoongozwa ndani ya sheria ya Agano la Yahweh ambalo alitoa kwetu kwa kuzudi hili.

Nimekuwa nikifunza Biblia kwa zaidi ya miaka 40 sio tu kwenye redio na runinga, lakini pia kupitia machapisho na mahubiri. Katika wakati huo, mara



kwa mara nimerejelea kwa Yohana 10:35. Kifungu hiki chenye kufundisha sana kinatuarifu, ***"Ikiwa aliwaita Elohim, wale waliojiliwa na neno la Yahweh (na maandiko hayawezi kutanguka)."*** Tunaweza kutangua Biblia, sio tu katika mistari, mlango au kitabu, lakini kwa maagano? Jana, nilizuru kituo cha kidini, na nikapata katika duka la vitabu, ikitolewa toleo la Pennsylvania Ditch la Agano Jipya, hivyo nikanunua juzuu hilo. Tayari niko na juzuu moja au mbili za Agano Jipya la Pennsylvania Dutch, lakini nilitaka juzuu hili haswa kwa sababu karibuni nitazungumza katika lahaja hii (au lugha, ukipenda) juu ya kisambazaji chetu kimpya kilichokuzwa cha redio ya mawimbi mafupi ya WMLK.

Niko katika mawasiliano na kundi linalochapisha majarida madogo katika palatinate katika Ujerumani. Mtu binafsi ambaye ni mhariri wa chapisho hili, aliandika mwaka mmoja au miwili iliyopita kwamba mkutano uliofanyika katika eneo la Palatinate la Ujerumani, uliohudhuriwa na wasomi 300 ambao walikuja kwa hitimisho kwamba lahaja hii ambayo wanaiita Palatinate German, ni lugha halisi. Ni lugha dada kwa *Hoch Deutch* ambayo ni Kijerumani cha juu. Lahaja hii pia ni lugha dada ya Yiddish kwa sababu, wale ambao wanaelewa Pennsylvania Dutch (Pennsylvania German) pia wanaweza kuelewa Yiddish vizuri sana. Mzungumzaji wa Yiddish katika Uyahudi pia anaweza kuelewa wale ambao wanazungumza lugha ya Pennsylvania Deutsch hapa katika sehemu ya mashariki ya Marekani na pia katika maeneo mengine, kwa mfano katika Indiana, Illinois, Missouri, nk., ambapo Amish walihamia.

Kwa sababu hiyo, nilinunua Agano Jipya la Pennsylvania Dustch, lakini kutumia Biblia nzima unahitaji kweli toleo la Kiingereza. Ninatumia Biblia ya **The Sacred Scriptures**, *Bethel Edition*, kwa sababu ya uhitaji wa kusahihisha idadi kubwa ya makosa yanayopatikana katika **King James Version**. Nilipoanza kusoma Maandiko Matakatifu zaidi ya miaka 40 iliyopita niligundua umuhimu wa kupata Biblia inayoonyesha nakala ya asili kwa karibu iwezekanavyo. Tulimaliza kuchapisha **The Sacred Scriptures**, *Bethel Edition* katika 1981 na tumemaliza kuchapisha tu uchapishaji wa sita, ambapo, wakati itakuwa imetawanywa kikamilifu, tutakuwa tumeweka zaidi ya kopi 30,000 mikononi mwa watafutaji wenye dhati wa kweli. Kati ya makosa 40,000 na 80,000 yameweza kusahihishwa kutoka kwa Biblia ya **Kings James Version** ikiwemo marejesho ya Jina la Mwenye-nguvu ambaye Jina lake ni Yahweh katika **Hebrew Bible** na Jina la Mwanawe ambaye ni Yahshua. Pia umeweza tu kunisikia nikisema neno *Elohim*. Tumerejesha neno *Elohim* kuchukua nafasi ya neno G-d (m-ngu), ambalo sio jina takatifu kabisa kulingana na nakala za asili (kwa karibu tuwezavyo kurudi kwazo).

Kama matokeo yake, ningependa kukuhimiza uzingatie njia sahihi ya kusoma Biblia, ambayo ni kuikubali Biblia nzima kutoka Mwanzo hadi Ufunuo kwa njia yako ya kutafiti Biblia. Nini hilo linamaanisha ni kwamba Jina la Mwenye-nguvu katika Agano la kale ni sawa kabisa kama katika Agano Jipya, ambalo linaweza kuthibitishwa kwa urahisi. Dr. Goerge Howard, wa chuo kikuu cha Geogia, ameandika nyenzo nyingi sana juu ya mada hii, akionyesha jinsi unaweza kwa kweli kusema mahali jina la Mwenye- nguvu liliweza kuondolewa kutoka kwa nakala kwa nukuu za Agano za kale ambazo zinaonekana katika Agano Jipya.

Nimekuwa nikizungumzia juu ya mada ya madarasa manne ya viumbe vilivyoumbwa ambavyo Mwenye- nguvu Yahweh aliumba kuwa watumishi wake. Anawaita binadamu *Obadiah, mtumishi wa Yahweh*, lakini pia aliumba viumbe vya kiroho, Makerubi na Maserafi. Tumechunguza mfanano na tofauti katika awamu zilizopita za mfululizo huu.

Sasa tumeanza kutafiti neno *Malachim*, ambalo ni la umbo la wingi la kiume la neno *ma'alak* linaloonyesha neno la kingereza *Malaika*. Darasa hili la viumbe vilivyoumbwa linaelezewa kwa umaarufu sana katika neno la Yahweh.

Umeweza kusoma kwamba kunaye Malaika maalum? Pia anajulikana kama MALAIKA MKUU. Alidhihirishwa katika sehemu kadhaa katika kitabu cha Mwanzo na alifanya sehemu muhimu katika tukio la kutoka Misri la taifa la Israeli. Tunasoma katika Kutoka 13:20, ***"Nao wakasafiri kutoka Sukothi, wakapiga kambi Ethamu, kwenye mpaka wa ile jangwa. Yahweh naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa nguzo, ili awaongoze njia, na usiku ndani ya moto mfano wa nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku; ile nguzo ya wingu haikuondoka mchana, wala ile nguzo ya moto haikuondoka usiku, mbele ya hao watu."***

Pengine umesikia maelezo mengi ya nguzo la wingu na moto, lakini ni nani aliyeonekana katika udhihirisho kwa wana wa Israeli? Kutoka 14:19, ***"Kisha malaika wa Elohim, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka akaenda nyuma yao; na ile nguzo ya wingu ikaondoka***

***hapo mbele yao, ikasimama nyuma yao."*** Kiumbe mwenye nguvu katika nguzo la wingu na moto sasa anaitwa Malaika wa Elohim; katika vifungu vya mapema, anaitwa Yahweh. Unaweza kupata maelezo tofauti kuhusu kiumbe huyu wa roho, kwani watu Wayahudi wanakataa Yule ambaye tunamwita Yahshua (malaika anayejitokeza katika Agano Jipya). Hata hivyo, maelezo ya msingi, na ya moja kwa moja ni kwamba malaika aliye na nguvu anaonekana katika nguzo la wingu na moto na anaitwa kwa Jina la Yahweh.

Kisha, tunapata katika mstari wa 20, ***"Ikafika kati ya jeshi la Misri na jeshi la Israeli...."*** Udhihirisho huu mkubwa uligawanya kati ya Waisraeli na Wamisri, ambao kwa haraka walikuwa wanawafuata Waisraeli, kujaribu kuwarudisha tena kwenye utumwa. ***"Napo palikuwa na lile wingu na lile giza, lakini lilitoa nuru wakati wa usiku, na hawa hawakuwakaribia hawa usiku kucha."*** Wamisri walikuwa kwenye giza, laikini Waisraeli chini ya ulinzi wa Yahweh, walikuwa na mwanga, kama ilivyokuwa imefanyika katika matukio mengine kadhaa.

Tunaendelea katika mstari wa 24, ***"Ikawa katika zamu ya alfajiri, Yahweh akalichungulia jeshi la Wamisri katika ile nguzo ya moto na ya wingu, akalifadhaisha jeshi la Wamisri."*** Ni wazi namna gani kwamba kulikuwa na kiumbe, ambaye alijitokeza katika nguzo la wingu na moto, ambaye kwa wakati fulani anaitwa Yahweh, na katika vifungu vingine, malaika wa Elohim. Kumbuka *Elohim* linamaanisha *mwenye- nguvu* (au wenye) au *Aliye na nguvu*. Ni nani Mwenye- nguvu wako? Ni nani aliye na mamlaka unayekubali kuamuru mapenzi Yake na matakwa yake kwako? Lazima ufanye uamuzi! Nimefanya uamuzi huo katika maisha yangu ya kibinafsi, kwamba Mwenye- nguvu Yahweh na Neno Lake atakuwa na njia huru katika maisha yangu kunifundisha na kunielekeza.




Ruhusu sasa tugeukie kwa Nehemia 9:9. ***"Tena uliyaona mateso ya baba zetu katika Misri, ukasikia kilio chao, huko kando ya bahari ya Shamu; nawe ukaonyesha ishara nyingi na mambo ya ajabu juu ya Farao, na juu ya watumishi wake wote, na juu ya watu wote wa nchi yake; kwa maana ulijua ya kuwa waliwatenda kwa kutakabari; ukajipatia jina kama vile ilivyo leo. Nawe uliipasua bahari mbele yao, hata wakapita katikati ya bahari katika nchi kavu; na wale waliokuwa wakiwafuatia ukawatupa vilindini, mfano wa jiwe katika maji makuu. Zaidi ya hayo ukawaongoza kwa nguzo ya wingu mchana; na kwa nguzo la moto usiku, ili kuwapa mwanga katika njia iliyowapasa kuiendea. Tena ulishuka juu ya Mlima Sinai, ukasema nao toka mbinguni, ukawapa hukumu za haki, na sheria za kweli, na amri nzuri na maagizo; ukawajulisha sabato yako takatifu, na ukawaagiza maagizo, na amri, na sheria, kwa mkono wa Musa mtumishi wako....Hata hivyo, wewe kwa wingi wa rehema zako hukuwaacha jangwani; nguzo ya moto haikuondoka wakati wa usiku, ili kuwaonyesha njia watakayoiendea. Pia, uliwapa roho wako mwema ili kuwaelimisha."***

Malaika maalum anaelezewa hapa. Malaika huyu maalum anatumia Jina Yahweh, LAKINI YEYE SIO YAHWEH ALIYE BABA, kwa sababu, katika Yohana 1:18, tunatambua kwamba hakuna aliyemwona Yahweh kwa wakati wowote. Mwana mzaliwa wa pekee, ambaye yuko kifuani mwa Baba, amemtangaza Yeye, kuifanye ijulikane kwetu jinsi tunavyoweza kuwa watoto wa kweli wa Yahweh.

Basi tugeukiwe kutoka kwa Kutoka 23:20. ***"Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengenezea. Jitunzeni, mbele yake, mwisikie sauti***

***yake; wala msimtie kisirani; maana, hatawasamehe makosa yenu; kwa kuwa jina langu limo ndani yake"*** Fikiria maana ya kifungu hiki. ***"Jina langu limo ndani yake"*** Baba anazungumza na Msemaji anawasilisha ujumbe. Anasema, "Jihadharini kwake, sikilizeni sauti Yake, ninazungumza kupitia Yeye, Jina langu liko katika Yeye; mamlaka na nguvu zangu zimewekwa ndani Yake. Unaweza kutambua kwamba Yeye ni Msemaji wa kweli, kwa sababu Jina Langu analolitumia (ambalo alitumia katika Agano la Kale) ni Jina Lake na utu Wake."

***"Lakini ukiisikia sauti yake*** [Msemaji] ***kweli, na kuyatenda yote ninenayo mimi***[mzungumzaji ambaye alikuwa Baba wetu wa Mbinguni, Yahweh Elohim]***; ndipo mimi nitakuwa ni adui wa adui zako, na mtesi wa hao wakutesao. Kwa kuwa malaika wangu atatangulia mbele yako, na kukufikisha kwenye Mwamori, na Mhiti, na Mperizi, na Mkanani, na Mhivi, na Myebusi; nami nitawakatilia mbali. Usiiwasujudie elohim zao, wala kuwatumikia; wala usitende mfano wa matendo yao; bali utaziangamiza kabisa, na nguzo zao utazivunja vipande vipande. Nanyi mtamtumikia Yahweh Elohim wenu, naye atakibariki chakula chako, na maji yako; nami nitakuondolea ugonjwa kati yako."*** (Kutoka 23:22-25).

Malaika anayeelezewa hapa anajulikana kama Yahweh, lakini kwa kweli ni Yahweh wa pili. Katika Zaburi 2:6, tunaambiwa, ***"Nami nimeweka mfalme wangu, juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu. Nitaihubiri amri; Yahweh aliniambia, ndiwe mwanangu, mimi leo nimekuzaa."*** Kwa kugeukia kwa Matendo ya Mitume 13:33, tunaambiwa kwamba Paulo anafunza jinsi andiko hili katika Agano la Kale lilitumika kwa Yahshua aliye Messiah. Atakuwa Mfalme. Yeye ni Messiah, Mtawala mkuu wetu sote, na amedhihirishwa kwa ajili ya wokovu wetu.

Katika Mwanzo 19:24, katika uharibifu wa miji ya tambarare, tunatambua kitu fulani cha maana sana. Lutu alikuwa ametolewa Sodoma, na alikuwa amekimbia kwa mji mdogo ulioitwa Soari (jina *Soari* katika Kiebrania linamaanisha *mdogo*). Tunasoma katika Mwanzo 19:23- 24, ***"Jua lilikuwa limechomoza juu ya nchi Lutu alipoingia Soari. Ndipo Yahweh akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa Yahweh."*** Unaona! Yahweh wawili wametajwa. Kunaye Yahweh mmoja mbinguni na Yahweh mwingine duniani. Kumbuka, katika Mwanzo 18, tunapata Ibrahimu akisimama mbele ya malaika huyu kuomba kwa uhifadhi wa Lutu na familia yake.

Mithali 30:4 inathibitisha yale nimekuwa nikikuambia. Sasa, kumbuka, tunageuka nyuma na mbele kupitia kwa Maandiko Matakatifu, kuoanisha Biblia kama tu Isaya 28:10 inatufundisha tufanye. Katika Mithali 30:4, tunasoma, ***"Ni nani aliyepanda mbinguni na kushuka chini?*** [Ni nani aliyefanya hilo] ***Ni nani aliyekamata upepo kwa makonzi yake? Ni nani aliyeyafunga maji ndani ya nguo yake? Ni nani aliyefanya imara ncha zote za nchi?*** [Ni nani aliyeumba mbingu na nchi] ***Jina lake ni Nani? Na ni gani jina la mwanawe, kama wajua?"*** Yahshua Messiah wetu alitimiza haya yote kama mwakilishi wa Baba Yake duniani, na alitimiza unabii huu.

Ninaamini kwamba jina la Mwenye-nguvu Muumbaji lilikuwa Yahweh Elohim. Hili ndilo tunaambiwa katika nakala ya Kiebrania. Pia ninaamini kwamba Jina la Mwanawe linajumuisha sehemu ya Jina la Yahweh, ufupisho wa jina la Yahweh kama linavyojitokeza katika neno HalleluYah (Yahweh). Unafahamu uhusiano? Jina la Kiebrania la Messiah ni Yahshua. Kwa sababu hiyo, "Jina langu liko ndani yake." Alikuja kutuokoa sisi, ambalo ni nini Jina Lake linamaanisha. Jina *Yahshua* linamaanisha *Yahweh ni wokovu*.

Je, maandishi na hekima ya Maandiko Matakatifu ni ya ajabu? Utafsiri wa kweli wa Maandiko ni wazi tunapomruhusu Yahweh kuzungumza kupitia Neno Lake. Nimefanya uamuzi kufuata Neno la Yahweh kama linatupea maagizo kuhusiana jinsi tunaweza kumkubali Yahshua aliye Messiah na mafundisho yake. Hautaweza pia kujifunza Ukweli zaidi wa Yahweh kwa kuwasiliana na Assemblies of Yahweh leo?

Andika kwa Assemblies of Yahweh, PO Box C, Bethel, Pennsylvania, 19507. Utakapotuandikia omba habari ya bei na jinsi unaweza kupata kopi ya biblia ya **The Sacred Scripture**, *Bethel Edition*. Utapokea kiasi kikubwa zaidi cha ufahamu wa ujumbe wa kibiblia kama unasikia sauti ya Baba wetu katika mbinguni akizungumza kwa kurasa za maandiko Yake matakatifu. SNB



# Vita, Njaa, na Mateteme

Basi tuzingatie baadhi ya vifungu vya Maandiko Matakatifu ambavyo vinashughulika na siku za mwisho, na kufunga kwa zama za binadamu. Mwenye-nguvu Yahweh yuko katika udhabiti wa unabii huu. Yahshua aliye Messiah, katika unabii wake wa mlima wa Mizeituni, ametuonya mapema kuhusu ukweli kwamba mwisho wa zama kutakuwa na vita na uvumi wa vita. ***"Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado."*** (Mathayo 24:6). Tunaweza kuona hili likifanyika kote kando yetu duniani, ambapo taifa moja linajiinua juu, dhidi ya taifa lingine na kutishia vita. Hatupaswi kuogopa, lakini lazima tutayarishe. Yahweh anatupa dirisha nyembamba la wakati kufanya kuitwa kwetu na kuchagulia hakika.

***"Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali. Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu."*** (Mathayo 24:7). Hatuwezi kuweka vichwa vyetu kwenye mchanga, kama mbuni wa kimethali anavyofanya, lakini lazima tukeshe na kuomba. Sasa ni wakati kujifunza jinsi ya KUMWAMINI Yahweh kwa mambo YOTE katika KILA NJIA. ***"Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Yahweh, ambaye Yahweh ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; hataona hofu wakati***



# eko ya Ardhi

***wa hari ujapo, bali jani lake litakuwa bichi. Wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda"*** (Yeremia 17:7-8).

Yahshua aliye Messiah katika unabii wake wa Mlima wa Mizeituni, anasema waziwazi ***"Amini, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia. Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe. Walakini, habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake."*** (Mathayo 24:34-36).

***"Mbingu na nchi zitapita: lakini maneno yangu hayatapita. WALAKINI HABARI YA SIKU ILE NA SAA HAKUNA AIJUAYE, HATA MALAIKA WALIO MBINGUNI, WALA MWANA, ILA BABA."*** (Mariko 13:31-32).

Katika kila ya unabii huu, Yahshua aliye Messiah anatahadharisha wasikilizaji Wake (leo, wale ambao wanasoma neno Lake) KUKESHA NA KUWA TAYARI. ***"KESHENI basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakapokuja mkuu wenu. Lakini fahamuni neno hili; kama mwenye nyumba angaliijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha, wala asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani mwana wa Adamu yuaja."*** (Mathayo 24:42-44).

